USHUHUDA WA UPORAJI WA ARDHI YA KIJIJI CHA BUYUNI DHIDI YA SERIKALI KATIKA MRADI WA VIWANJA 20,000 KATIKA MKOA WA DAR-ES-SALAAM.

1. UTANGULIZI

Kijiji cha Buyuni kipo kusini magharibi mwa Jiji la Dar-es-Salaam; katika Kata ya Chanika, Tarafa ya Ukonga, Wilaya ya Ilala katika Mkoa wa Dar-es-Salaam. Kijiji hiki kilianzishwa mwaka 1975 na kuandikishwa rasmi mnamo tarehe 24/3/1980 na kupewa Hati ya kuandikishwa yenye Na. 43.

2. MATATIZO YA ARDHI KWA WANAKIJIJI WA BUYUNI

Mnamo mwezi Septemba mwaka 2002 Serikali ilibuni mradi wa viwanja 20,000 katika mkoa wa Dar-es-Salaam. Mradi huo ulianzishwa katika Vijiji mbalimbali vya mkoa wa Dar-es-Salaam, vikiwemo Vijiji vya wilaya ya Ilala, Temeke na Kinondoni.

Kijiji cha Buyuni ni miongoni mwa kijiji kilichopatwa na janga hilo.Hivyo mnamo mwezi Septemba mwaka 2002 Wataalamu toka Wizara ya Ardhi nyumba na maendeleo ya makazi wakishirikiana na viongozi na wataalamu toka Manispaa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya walifika kijijini na kuandaa mkutano wa hadhara na kutueleza kwamba Serikali imeamua kuchukua ardhi yetu ya kijiji ili kupimwa viwanja 5,000 kati ya viwanja 20,000.

Hivyo mkutano huo ulitoa maelezo yenye maagizo kwamba viwanja hivyo lazima vitapimwa kwa agizo la serikali na siyo hoja za wananchi. Hali hiyo ilisababisha mvutano mkubwa kati ya serikali na wananchi wa kijiji cha Buyuni ambao walipinga vikali dhuluma hiyo. Baada ya hapo Wanakijiji waliamua kuunda kamati ili kufuatilia zaidi katika kudai haki zao za kimsingi. Ilipofika tarehe 25/10/2002 Wanakamati wa kijiji cha Buyuni na Wanakamati wa vijiji vingine vilivyokuwa katika mradi huo, kwa pamoja waliamua kuungana na kuandaa Tamko la Malalamiko kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kupinga mradi huo hatari wa ambao kimsingi haukuwa na maadalizi ya kutosha.

Lakini pamoja na harakati zote hizo za kupinga zoezi hilo ambalo halikushirikisha Wananchi, Serikali iliamua kutumia nguvu zake za dola na kutwaa ardhi ya Wananchi bila sababu ya msingi ya kisheria. Hivyo tarehe 11 Novemba, 2002 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliamua kutwaa ardhi ya Wanavijiji wanyonge na walalahoi bila kujali athari zitakazowapata wanavijiji hao wakiwemo Wanawake, Watoto na Wazee, ambapo ardhi hiyo siku za nyuma za operesheni vijiji waliamishwa katika makazi yao ya asili na kupelekwa katika Vijiji vya Ujamaa. Lakini leo tumeshuhudia serikali ikipora ardhi hiyo bila ya utaratibu na kuwaacha Wananchi wakitangatanga na hawajui watakwenda wapi.

Hivyo baada ya majibu ya Tamko hilo toka kwa Rais, vyombo vya dola na watawala wake katika ngazi mbalimbali walitumia vitisho dhidi ya Wananchi ili wakubali amri hiyo, na yoyote atakayopinga amri hiyo angekamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria. Hivyo ndivyo hali halisi ilivyokuwa katika Kijiji cha Buyuni katika kufanikisha uporaji ardhi ya Wanakijiji.

3. HASARA ZILIZOJITOKEZA KATIKA MRADI HUO KWA KIJIJI CHA BUYUNI.

(a) Hasara zilizojitokeza kwa Kijiji;

- Hivi sasa hali ya kiuchumi imekuwa mbaya siyo kama ilivyokuwa pale siku za nyuma, ingawa serikali ilisema kupimwa viwanja kutaleta maendeleo ya haraka kwa wanakijiji wa Buyuni. Wananchi wengi walipoteza vyanzo vyao vya kuwaingizia kipato
- Wananchi wengi waliokuwa wanaishi katika eneo hilo la mradi wameamua kuhama kabisa na kuhamia sehemu nyingine za mkoa wa Pwani, baada ya kushindwa gharama za ununuzi wa viwanja katika eneo hilo la mradi.
- Sehemu kubwa ya eneo lililochukuliwa kwa hivi sasa limekuwa pori ambalo linatishia usalama wa mali na maisha ya wananchi waliobaki kwani ni maficho ya wahalifu na hata wanyama hatari wanaweza kujificha humo

- Eneo hilo kwa hivi sasa halina shughuli zozote za maendeleo na kumesababisha wananchi kuvamia msitu wa hifadhi wa Kazimzumbwi na kukata mkaa na miti ya kujengea ili kupata fedha za kujikimu kwa maisha yao ya kila siku.
- Kumekuwa na mgawanyiko kati ya viongozi wa kijiji na wananchi na kujenga chuki dhidi ya serikali.
- Wanakijiji waliobaki hawana uhakika na maisha yao na mali zao, kwani kijiji kizima cha Buyuni kimevamiwa na miradi mbalimbali ikiwepo ile ya Uwanja wa ndege,Manspaa na Kanisa jipya la mitume
- Kutokana na uporaji huo wa ardhi kijiji hicho kimefikia kupoteza sifa za kuwa kijiji, na hivi sasa kimetangazwa kuwa eneo la mji katika Manispaa ya Ilala

(b) Hasara zilizojitokeza kwa mwanakijiji mmoja mmoja;

- Baadhi ya familia zimepoteza maeneo ya kuishi na hazina uhakika wa kupata maeneo mbadala
- Wengi wa wanakijiji wamepoteza ajira zao za kila siku ambazo ni kilimo cha mazao ya chakula na biashara.
- Wanakijiji wengi hivi sasa wanashindwa kuwasomesha watoto wao katika elimu ya sekondari kwa sababu mali zao walizokuwa nazo tayari zimechukuliwa.
- Baadhi ya wanakijiji wanashindwa kujikimu kwa chakula,matibabu na hata malazi
- Shughuli za kila siku za kiuchumi zimevurugika.
- Wanakijiji wengi wameamua kuhamia wilaya ya Kisarawe na wilaya ya Mkuranga huko mkoani Pwani baada ya kushindwa kabisa kuendesha maisha yao ya kila siku katika kijiji cha Buyuni.

4. HARAKATI ZA WANAKIJIJI WA BUYUNI WALIVYOKATAA KUBURUZWA.

Mnamo mwishoni mwa mwaka 2000, Wanakijiji wa Buyuni walishuhudia uvamizi wa kuporwa ardhi kwa mara ya kwanza, zoezi lililoendeshwa na Manspaa ya Ilala. Zoezi hilo lilikuwa la upimaji viwanja lililoendeshwa na kampuni iitwayo Majengo Dynamic Survey toka jijini D'Salaam iliyokuwa chini ya udhamini wa Manspaa ya Ilala. Upimaji huo ulihusu viwanja vya makazi kwa watu wa Kipawa na upimaji wa sehemu ya kiwanda cha kuharibu vyakula vilivyokwisha muda wake kutumika.

Zoezi hilo liliharibu mazao ya wanakijiji na baadhi ya vibanda vyao, na kibaya zaidi zoezi hilo halikushirikisha Wanakijiji wala Viongozi wa kijiji. Baada ya tukio hilo lililowakera Wanakijiji kwa pamoja waliunda kamati na kufuatilia ngazi mbalimbali ikiwemo ile ya Kitongoji, Kijiji,Kata hadi Wilaya.Na ndipo mnamo tarehe 28/11/2000 alikuja Katibu Tarafa kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya na kusema kwamba anaomba radhi sana kwa kosa hilo la kuvamia. Hivyo aliwaomba wanakijiji wasubiri hadi hapo Mkuu wa wilaya atakapokuja, pia alisema zoezi hilo linahusu katika kijiji cha Pugu-Kajiungeni katika eneo la Kinyamwezi na siyo kijiji cha Buyuni.

Baada ya ukimya wa muda mrefu, Kamati iliandaa vikao vya aina mbalimbali ili kujua nini kinaendelea juu ya haki yao na kuwaunganisha wanakijiji wenzao. Na ilipofika tarehe 13/8/2001 Afisa mtendaji wa kata ya Chanika aliwaleta Wathamini ili waje wathamini mali za wananchi.Baada ya hoja hiyo wanakijiji kwa pamoja walipinga vikali kuthamini mali zao na wakaamua kuwafukuza kabisa watu hao.

Na ilipofika tarehe 10/2/2002 Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya alikuja katika mkutano wa hadhara hapo kijijini na kutoa madhumuni ya upimaji huo wa viwanja. Kwa kuwa huko nyuma katika vikao tulivyokutana vilikuwa havina ukweli , Wanakijiji kwa umoja wao walipinga kauli hiyo ya Mkuu wa wilaya ya Ilala na kusema hawataki kabisa kuporwa ardhi yao ya kijiji bila ya kushirikishwa,kwani wao ni wananchi wa nchi hii ya Tanzania wanayo haki ya kuhoji haki zao kisheria.

Baada ya kauli hiyo Mkuu wa Wilaya alitoa vitisho kwa wananchi na kudiriki kusema kwamba yeye pamoja na Serikali ni Paka na sisi Wanakijiji ni Panya hatuna ujanja wowote ule, chochote kile wakitaka watafanya bila kujali mtu yoyote yule. Pamoja na kauli hiyo ya vitisho Wanakijiji wa Buyuni hawakuyumba na kwa pamoja walisema hawataki na hawatatoa ushirikiano wowote ule wa kuporwa mali zao.

Hitimisho

Harakati hizi za wanakijiji wa Buyuni zinatufudisha mambo mengi. Kwanza, kwamba katika karne hii ambayo serikali ya Tanzania inahubiri siasa za utawala bora na utawala wa sheria, bado yenyewe ndio inayoongoza kwa kukiuka misingi ya utawala bora na sheria. Wananchi wa Buyuni hawakushirikishwa karika maamuzi ya msingi yanayowahusu. Na hii ni kielelezo tu kwamba wananchi wengi wanaporwa haki zao kwa vile tu watawala hawataki kuwasikia wanasemaje hata pale uamuzi unapofanywa kuhusu mali na rasilimali zao

La pili, tumeona jinsi silaha ya mnyonge ilivyoendelea kuwa umoja wake. Wananchi wa Buyuni wasingeungana pamoja na kukataa kuburuzwa, bila shaka maamuzi mengi ya hatari yangeshafanyika juu yao na juu ya ardhi wanayoitumia.

La tatu, tumeona pia kuwa haki haiwezi kupatikana bila harakati za kuidai na kuifuatailia kwavile wenye mamlaka wamejijengea kawaida ya kuhodhi maamuzi juu ya haki za wananchi.

Nne, suala zima la upanukaji wa miji na mipango miji linapaswa kuangaliwa upya kwani imekuwa kawaida miji inapopanuka kumeza haki za wananchi hasa wale wanaomiliki na kutumia ardhi kimila pembezoni mwa miji hata kama umiliki wao ni wa halali. Wananchi wa Buyuni ni kiwakilishi cha wananchi wengi sana waishio pembezoni mwa miji ambao haki zao hufinyangwa na wenye mamlaka ya kusimamia haki hizo hasa mamlaka za mipango miji.

Suala la haki za kimila kulindwa na sheria sawa na haki za sheria ni la muhimu sana kwasababu wananchi wengi waishio vijijini na hasa pembezoni mwa miji wamekuwa wakipoteza haki hizo wakati fulani sheria zikiwalinda wavunja haki. Ifikie wakati sheria ziwalinde pia wamiliki wa ardhi za kimila kama zinavyowalinda wamiliki wengine.